

## Maswali

1. Paulo alikuwa na ndugu wangapi kwa kikundi chake?
2. Walikuwa wanapeleka nini Yuda?
3. Paulo na Luka walikuwa wapi kabla ya Troa?
4. Ni siku gani ya juma hawa watu walikutana na waumini kule mjini?
5. Paulo alizungumzia juu ya kitu gani hasa?
6. Mkutano ulichukuwa mda gani?
7. Mbona Eutiko alianguka?
8. Paulo alifanya nini?
9. Waumini walifanya nini baada ya hayo?
10. Nini ilifanyika wakati Paulo na kikundi chake walikuwa wakitoka?

## Majibu

1. 8
2. Walikuwa wanapelekea ndugu na dada waliokuwa maskini pesa kule Yuda.
3. Walikuwa wamekuwa Filipi.
4. Jumapili jioni.
5. Labda Paulo alizungumzia juu ya kuwa na imani kwa Kristo na kujihadhari na ndugu waongo.
6. Mkutano ulikuwepo usiku kucha.
7. Alianguka kwa sababu alikuwa analala.
8. Paulo na wengine walienda haraka alikokuwa Eutiko.
9. Baadaye walimega mkate na kunywa divai.
10. Kulipokucha, Eutiko aliletwa ndani ya chumba akiwa hai na mzima.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

### Awamu ya 1 Mwaka wa 2



# 51 Eutiko analala

## Marejeo

Matendo ya mitume 20:6-12

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Paulo alikuwa na uwezo wa kufanya miujiza

## Maneno maalum


1. Troa + kikundi + pesa
2. Safari
3. Jumapili + Eutiko
4. Paulo anazungumza + uaminifu + hatari
5. Usiku wa maneno + usingizi + anguka + ngazi
6. Maishani + mkate na divai + jua lilichomoza
7. Tembea + shukrani + kutoka kwa wafu

**51.1** Paulo alipokuwa kwa safari yake ya mwisho, alifika Troa mji mmoja ya miji za nchi ya Uturuki. Tunasoma ujumbe wa Yesu kwa kitabu cha ufunuo kuhusu kanisa la Efeso na zinginezo. Katika kikundi cha Paulo kulikuwa na wandugu wengine wanane. Unaweza kusoma majina na Eklesia kwa kitabu cha Matendo ya Mitume 20:4. Labda walikuwa na pesa nyingi. Hii ilikuwa changisho waliyotowa Korintho na Makedonia kupelekea ndugu na dada walioko Yudea.

**51.2** Wengi wao walikuwa wako Troa wakati Paulo na Luka walifika kule. Walitoka Filipi na wakafika Troa baada ya Pasaka. Safari yao ilichukuwa siku tano.

**51.3** Walikaa Troa karibu juma moja. Walinua kuendelea na safari ili wafike Yudea na Yerusalemu Jumatatu. Jumapili yaani siku moja kabla waondoke, walikuwa na mkutano mjini na waumini. Kulikuwa na kijana mmoja jina lake Eutiko aliyekuwa amekaa kwa dirisha la orofa. Alikuwa akimsikiliza Paulo.

**51.4** Paulo alikuwa na mengi ya kuambia watu. Hatujui alichosema lakini tunaamini aliwaambia wawe na imani kwa Yesu hata nini ifanyike. Tunajua Paulo aliwahatarisha ndugu wa Efeso kuhusu wandugu waongo. Efeso haikukua mbali na Troa kwa hivyo labda alisema maneno mamoja huko. Ingawaje kwa kitabu cha Ufunuo hakuna barua yenye Yesu aliandikia watu wa Troa. Labda hakukuwa na Eklesia Troa baada ya miaka thelathini.



**51.5** Mkutano uliendelea jioni yote mpaka usiku wa manane. Taa ziliwaka vizuri. Eutiko aliyekaa kwa dirisha alianza kuchoka. Labda moshi kutoka kwa taa na joto iliyokuwa chumbani ilimfanya achoke. Au ni kwa sababu alikuwa kijana na amekuwa na usiku mwingi na shuguli nyingi bila kulala. Alianza kulala hapo juu ya dirisha na mara tu akaanguka chini kutoka juu. Kutoka juu mpaka chini alikoanguka ilikuwa futi 20. Alikufa alipoanguka. Mazungumzo yalikatishwa papo hapo. Paulo na watu wengine waliteremka gizani haraka haraka kuona vile Eutiko alikuwa.

**51.6** Paulo aliwambia, "Msijali kuna uhai ndani yake." Paulo alilala juu ya Eutiko na kumkumbatia. Paulo alijua kwamba Mungu atafanya muujiza. Paulo alirudi kwa mkutano na akaendelea na mazungumzo. Walikuwa na meza ya Bwana kwa kumega mkate na kunywa divai. Walishukuru Mungu kwa kuleta Yesu awe dhabihu ya kuokoa wote wanaomuamini. Mkutano uliendelea mpaka jua likatoka.

**51.7** Wakati Paulo na watu wake walipokuwa wakijitayarisha kutoka, Eutiko alingia chumbani walikokuwa. Alikuwa hai na mzima. Kila mtu alipomuona alifurahi na kushukuru Mungu kwa kumrudishia uzima kutoka kwa wafu.

